# Mapinduzi Ya Nne Ya Viwanda na ufanyaji wa biashara Tanzania; Tumejipangaje?

Mada katika Mkutano wa Brela na Wadau, Tarehe 27 Oktoba, 2023, Mlimani City, Ikitolewa Na

Daktari, Eve Hawa Sinare,Wakili, EhLaw Research Advocates

# TUMEJIPANGAJE

- "Urasimishaji wa Biashara katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda" unazingatia matumizi ya teknologia katika utaratibu mzima wa kusajili makampuni na majina ya biashara. Haya mapinduzi yalishafika BRELA tangu mwaka 2018 ilipoanzishwa mfumo wa Online Registration System ( ORS), mfumo ambao umewezesha wadau kusajili kampuni au jina la biashara bila kufika ofisi za BRELA.

Faida ya mapinduzi ya utaratibu:

- Kuokoa muda na kero za kupanga foleni ofisi ya BRELA
- Kuokoa gharama ya watoa huduma,, hasa mawakili, kwa wateja ikiwa ni malipo ya huduma na ya gharama za kufuatili usajili
- Kupunguza kero ya taarifa za makampuni au majina ya biashara kutokuwa kamilifu kutokana na kutokuwepo kwenye mafaili husika
- Upatikanaji wa taarifa kwa urahisi zaidi na zenye uhakika zaidi

Mapungufu ambayo yamejitokeza katika miaka 5 tangu mfumo wa ORS kuanzishwa:

- Kujisajili kama mtumiaji wa ORS kunahitaji kitambulisho cha Taifa; wakati wapo watanzania wengi ambao hawana vitambulisho vya taifa kwa sabababu mbalimbali. Hali hiyo inawanyima wadau wengine fursa ya kujisajili na kutumia mfumo wa ORS.

- Baada ya Kujisajili, Mfumo hudai mabadiliko ya password mara kwa mara hata wakati kwa mtumiaji hata muda haujapita mrefu wa kustahili kubadili password;
- Wakati wa kutumia kwa muda, mfumo hudai “time expired” na kujifunga. Mtumiaji anaweza kupoteza “data” zilizoingizwa na kulazimika kuanza upya. Hii inampotezea mtumiaji muda na kero ya kuanza upya;

Wakati wa kusajili kampuni, kuna changamoto kadhaa, kubwa zaidi ni kama zifuatavyo:-

- Orodha ya kazi/shughuli za kampuni iliyo kwenye Mfumo haina maelezo ya kutosha, na mfumo hautoi nafasi ya kueleza ili kutosheleza yaliyo kwenye "Memorandum and Articles of Association". Mtumiaji analazimika kuchagua maelezo mafupi-mafupi yaliyo kwenye orodha ya kazi/shughuli ambayo mara nyingine hayaendani na Object clause halisi ya kampuni. Mwisho wake "Consolidated Company Form" inakuwa ndefu na sio sahihi kwenye Objects.

- Kuna haja ya kurejea hii sehemu ya mfumo nia ikiwa kuwezesha mtumiaji kueleza main object clause ya kampuni bila kuwa na mesto wa kuchagua. Kusiwe na sample memorandum of association au articles of association. Sheria ya makampuni ina mfano wa articles of association ambayo inampa makampuni uhuru wa kufanya mabadiliko kadhaa. Kinachotakiwa BRELA kwenye sehemu hii ni kumtaka mtumiaji aandike main objects ya kampuni tu.

- Kwenye kuingiza Kiasi cha Mtaji kilichoidhinishwa na idadi ya hisa pangefanyiwa maboresho ili pawe rahisi zaidi kwa matumizi (user friendly)

- Kwenye uchaguzi wa mtu mwenye kibali cha kufanya marekebisho yoyote kwenye Kampuni kupitia mfumo wa ORS siku hizi haukubali uteuzi wa mtu asiye mkurugenzi, jambo linaloleteleza mahangaiko kwa wenye kampuni, kwani si lazima mwenye kampuni/mkurugenzi ajue jinsi ya kujiandikisha na hatimaye kutumia mfumo. Makatibu wa Kampuni, (company secretaries ndiyo walio na jukumu lafiling compliance pamoja na wasaidizi wao kuhakikisha filing, wanasheria wanaotoa huduma kwa wawekezaji wangeweza kuongezwa kutumia ORS system kwa kampuni husika. Ingeongeza idadi ya watumiaji wa mfumo. Ikumbukwse kuwa wenye makampuni au wakurugenzi sio wanaotegemewa kutumia mfumo.

- Umuhimu wa taasisi zinazotoa huduma ya usajili na baada ya usajili kuaminiana katika kudai documents.
- BRELA ndio ina nakala halisi (original) memarts za kampuni na cheti uhai cha kampuni (Certificate of Incorporation) au cheti cha kusajili cha jina la biashara ( Certificate of Registration). Isingehitajika tena TRA, au Halmashauri kwa leseni za biashara zinazotolewa kwenye Halmashauri, kudai nakala za memarts au Certificate of Registration au kwa makampuni kudai nakala za memarts. Yaani kuna duplication ya documents sana kitu ambacho hakina tija.

- Kama mtumiaji anahitaji kupata certified copy of the memart inabidi alipe TZS3,000 kwa kila page (ukurasa). Ingekuwa afadhali kudai hela ya jumla ya shillingi elfu 10 kwa huduma kuliko kudai kwa ukurasa. Ingekuwa ni huduma sio njia mojawapo ya kupata pesa.
- Miaka ya 1996/97 serikali iliondoa gharama za kusajili kampuni kwa kufuatia na kiasi cha authorised share capital ambayo haiendani na kiasi cha uwekezaji au uwezo wa mwekezaji,.

- Sasa mwekezaji anaweza kulipa zaidi ya laki nne kwa gharama ya usajili kama ( authorized share capital) imezidi shilingi milioni 50. Ingefaa kurudi kwa kudai gharama moja ya kusajili na gharama iwe kiasi kisichokuwa kikubwa ili kuhamasisha wafanya biashara kujirasimisha chini ya sheria ya Makampuni

# Mabadiliko ya sheria ya makampuni ambayo hayako rafiki kwa uwekezaji kwa kutumia makampuni

Kumekuwa na mabadiliko kwenye sheria ya Makampuni ambayo yamekingana na vipengele vya Katiba, na sera ya uchumi ambayo ina lengo la kutumia sekta binafsi kama injini ya kurudumu la kukuza uchumi na kukingana na sheria yenyewe ya makampuni. Hapa muda hautoruhusu kutaja vifungu vyote ila nitazungumzia vichache tu.

- ❑Section 400A
- ❑Uwajibikaji wa wakurugenzi kwa kampuni na nje ya kampuni
- ❑Section 16(2)

# Section 400A

- Section 400A of the Companies Act-TLS ilipendekeza ifutwe kwa kuwa inakingana na Katiba, inakingana na basic principle ya sheria ya makapuni kuwa liabilities na assets za kampuni ni za kampuni na haichanganyiki Kwenda kwenye wanahisa au wakurugenzi, inakingana na sheria ya muda mrefu ambayo imewekwa kwenye sheria yetu ya makampuni kuwa wakurugenzi wapo responsible kwa kampuni, na wakati mchanhe kwa wanahisa na wafanyakazi na pia iko discretionary. Hii ibara ililetwa na mabadiliko ya sheria Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Act of 2019
- Hii ibara inafanya kufanya biashara kwa kutumia kampuni kuwe hakuna tofauti na kufanya biashara kwa kutumia jina binafsi au jina la biashara. Haina faida kwa kuwa nia ya kutumia kampuni ni ku-limit liabilities ambazo mwanahisa au mkurugenzi wa kampuni anaweza kupata. Hiki kipengele kimeondoa tofauti kati ya mwanahisa na kampuni

- Ibara hii inamruhuru Msajili wa makampuni kuondoa jina la kampuni ambayo  inafanya biasharai kwenye rejista kama akiwa na sababu ya kuamini kuwa moja au zaidi ya makosa yalioorodheswa yamatokea. Makosa yalioorodheshwa mengine ni ya jinai na standard ya kutumia kwenye makosa ya jinai ni "beyond reasonable doubt" Msajili atatumia "reasonable ground to believe"  kwamba kosa limefanyika kwenye mambo ambayo ni ya jinai wakati kigezo cha makosa ya jinai ni " beyond reasonable doubt".

- Kufuatana na hali halisi ya  kazi za usajili, msajili hawezi kuhisi kuwa kosa kati ya yalioorodheshwa limefanyika ila tu kwa kuambiwa na agency ingine ambapo ni kinyume na ibara yenyewe ambayo inategemea Msajili agundue kutokana na kufanya kwake kazi ya usajili,
- Mwenye kampuni atafahamu kuwa kampuni imefutwa kwenye rejista baada ya kampuni kuondolewa kwenye rejista. Hata kama anaweza kwenda mahakamani   baadaye jina likarudishwa tayari hasara imeshatokea.

- Ibara inamuadhibu mtu ( kampuni inayofutwa) kwa kosa ambalo limefanywa na mtu mwingine, kinyume na kanuni msingi kuwa adhabu anapewa aliyekosa.
- Mfano mwenye kampuni au wakurugenzi wanaweza kufukuzwa Tanzania (PI) basi kampuni itafutwa jina. Lakini aliyekosa sio kampuni.
- Kwa nini serikali isitumie investment termination clause kwenye wawekezaji wa nje na kulazimisha kampuni kama wawekezaji ni wa ndani watanzania kufunga biashara waweze kuuza mali ya kampuni, walipe madeni na kuzika kampuni?

- Ibara haikuzingatia haki za watu wengine kama- ( employees, creditors secured or otherwise; chain suppliers, service providers, shareholders, the public, and the economy might be affected). Jina likiondolewa kwenye rejista basi kampuni inasimamisha shughuli, mikopo yake yote inakuwa imeiitwa, na haiwezi hata kuanza utaratibu wa ufilisi au kuuza mali ili illipe madeni.
- Hii haijalishi kampuni ni kubwa kiasi gani Ibara haikuweka kipengele cha kuokoa matendo ambayo kampuni imefanya huko nyuma kama ikifutwa kwa kosa linaloendana na incorporation. Kila ililofanya huko litakuwa batili

- Haieleweki kama kampuni ina ruhusiwa kuanza ufilisi wa kampuni ambayo jina limeondolewa kwenye rejista kwa kuwa haitaruhusiwa kutumia jina kwa njia yeyote tena baada ya kufutwa na mali za kampuni zitaangaliwa na nani. Hii ni kinyume na ibara 24 ya Katiba inayowajibisha Serikali kulinda mali za watu wakiwemo makampuni. Ibara inachukua mrengo wa the loss lies where it falls. Msimamo kama huo hauhamasishi watu kuwekeza kwenye nchi yetu wawe wa nje hata wa ndani.

- Hii itawaumiza wafanya biashara na makampuni ya ndani. Makampuni ya nje wataweza kudai Tanzania gharama za mali zao na hasara nyingine zinazohusika kwa kutumia international principle of expropriation ambayo itairuhusu kampuni kusaka mali za Tanzania popote mpaka alipwe. Hii ibara inaumiza makampuni ya ndani ya watanzania. Vigumu mtanzania akamate mali za Tanzania nje ajilipe kisha aendelee kufanya biashara hapa.

- Hii ibara imeigwa kutoka continental Europe lakini ikawekwa kinyume na wanavyofanya. Kule sababu ni nyingine na uamuzi ni wa mahakama. Mfumo wa sheria za Tanzania ni wa Common law ambao unapendelea kama kampuni inahitaji kufutwa basi iwekwe kwenye ufilisi na kuna utaratibu ambao unajulikana kuhusu wakopeshaji, wadai wengine na wakopeshaji ambao hawana dhamana (security) na jinsi gani kuzika kampuni. Ibara hii hata haijaweka kampuni itakufa je (dissolved)

# Kuwajibika kwa wakurugenzi (Directors liabilities)

- Sheria ya makampuni imeweka wazi kwenye ibara Ibara ya 181 inawapa majukumu directors kuendesha kampuni kwa biashara na kuitaratibu. Ibara182-185 inaweka ukomo wa uwajibikaji kwa wakurugenzi kwa kampuni kwa jinsi wanavyoendesha kampuni, kwa wanahisa na kwa wafanyakazi. Imeweka kikomo cha liability kwa wakurugenzi kwa wanahisa kwa kuwa kuna tofauti kisheria kati ya kampuni na wanahisa wake kwenye kwa mali na liabilities za makampuni. Ibara 400A na sheria nyingine nyingi zimewawajibisha directors criminally kwa madeni au makosa ya kampuni, au kwa non- compliance kinyume na ibara 182-185.

- Kampuni kama mtu wa kisheria mwenye utu kama mtu na kuwa na uwezo wa kuwa na mali na madeni, kuwa na mikataba na kushtakiwa au kushtaki ilikuwa na nia kuwa wawekezaji waweze kuchukua risks wawekeze kwa kutumia kampuni na kama uwekezaji ukifeli basi mwekezaji hatofilisiwa mali yake yote  ili kulipa madeni.  Madeni yote ya kampuni yanakuwa limited kwa shares. Ndiyo maana kampuni zinaitwa limited liability companies kwani ndiyo aina ya kampuni inayotumiwa.

- Ndiyo maana liability ya makampuni ni limited. Hizi sheria zinazowapa directors na shareholders liability za makampuni zinakiuka misingi muhimu ya lengo la sheria ya makampuni. Watu wenye uwezo wa kuendesha makampuni watakuwa hawatotaka kuwa wakurugenzi. Na kwa kawaida ni kitu ambacho hakifanyiki kwenye nchi nyingine za Common Law. Pia vinakingana na vipengele vilivyoko kwenye sheria ya makampuni inayolimit liability za madirectors.

- Hii ni tatizo kubwa kwa wawekezaji wa nje na wa ndani lakini haswa wa nje. Wataogopa kuja kuwekeza kama wanahofu directors wataweza kudaiwa madeni ya makampuni na kuwekwa ndani na kuwa na kesi za jinai. Country risk inakuwa kubwa. Watakaokubali watadai investment  insurance kubwa sana.
- Tanzania irudi kutambua umuhimu wa kutenganisha kampuni na wawekezaji juu ya mali na madeni ya kampuni kama ilivo kwenye nchi nyingine.

# Kufuta share warrants Tanzania

- Finance Act of 30th July 2021 ilibadilisha kipengele cha ( section) 85 cha sheria ya makampuni kukataza kampuni yeyote kutoa share warrants na kuweka mazingira ya watu ambao walikuwa na share warrants kuziwakilisha kwenye makampuni yao.
- Mabadiliko hayo yana impact kwa kanuni zilizowekwa za GN No. 478 ya tarehe 21/7/2023 Companies Beneficial Owners) Regulations 2023. Kuna haja ya kurejea kanuni upya na kuangalia ulazimu ya matakwa mengine yalioko

## Msajili asajili kampuni kama taratibu zote zimezingatiwa- implication za kufutwa section 16(2)

- Kipengele cha 14(4) cha sheria ya makampuni kinamuwajibisha Msajili asikubali kusajili kampuni yeyote kama hana uhakika kuwa taratibu zote za usajili wa kampuni husika umefuatwa itakiwavyo
- Msajili hayupo karibu na matayarisho au karatasi na taarifa za kampuni inayotafuta kusajiliwa

- Kipengele cha 16 (2) cha sheria ya makampuni kilimpa jukumu la kutoa kiapo wakili atakayetayarisha makaratasi ya kampuni kama memorandum na Articles of association atoe tamko la kiapo kuwa taratibu zote na karatasi zote zinazotakiwa chini ya sheria  zimefuatwa.

- Inampa kivuli Msajili kusajili kampuni bila kufikiria kuwa taratibu hazikufuatwa kikamilifu. Bahati mbaya mabadiliko ya sheria chini ya Finance Act No. 8 ya 2020 ilifuta kipengele 16 (2). Sasa Msajili husajili bila mwavuli wa declaration ya compliance. Hii ianondoa nia ya kulinda uhalisi wa uhai wa kampuni kuepuka wakati wowote jina la kampuni lisifutwe.

# conclusion

- Bado kuna mabadiliko mengine kwenye sheria ya makampuni ambayo muda hauruhusu kuzitaja, na sheria nyingine nyingi ambazo zinagusia mambo ya biashara na uwekezaji.
- Nimalizie kwa kusema kweli BRELA imepiga hatua kubwa katika kudigitilise huduma. Imeleta mafanikio mengi makubwa. Kinachobakia baada ya miaka 5 tangu mfumo kuanza ni maboresho tu ya mfumo na wa sheria ya makampuni na ya majina ya biashara.

Asante Kwa kunisikiliza